Ufugaji>>

MWANANCHI UK 17.

# *Serikali yahimiza matumizi chanjo ya mifugo*

Hadija Jumanne, Mwananchi
hjumanne@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Riziki Shemdoe amewataka wafugaji kote nchini kuacha kufuga kwa mazoea, badala yake wazingatie matumizi sahihi ya chanjo za mifugo zinazozalishwa na Serikali.

Profesa Shemdoe alisema hayo juzi, wakati wa ziara yake kutembelea Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) ambapo alisisitiza kuwa matumizi sahihi ya chanjo yataleta uhakika wa soko la nyama ya Tanzania nje ya nchi.

"Serikali imekuwa ikitoa fedha hapa kwa ajili ya kuongeza vifaa na kuzifanya maabara zetu ziwe za kisasa zaidi, tutaendelea kuiangalia TVLA kwa jicho tofauti, kwani ni eneo ambalo tukiliimarisha mifugo yetu itapata masoko mengi ya nje ya nchi," alisema.

Alisema miaka ya nyuma Tanzania ilikuwa inauza nyama nje ya nchi tani 1,000 kwa mwaka, lakini katika kipindi cha mwaka 2021/2022 idadi hiyo imeongezeka hadi tani 12,000.

Awali akiwasilisha taarifa kwa Katibu Mkuu huyo, Mtendaji Mkuu TVLA, Dk Stella Bitanyi alisema katika kipindi cha miaka sita kuanzia 2016/2017 hadi 2021/2022 TVLA imezalisha jumla ya dozi 325,979,034 za chanjo za mifugo.

Dk Bitanyi alisema ili kuleta tija kwa nchi, TVLA wataendelea kufanya kazi kwa weledi ili kutoa huduma bora na kuipeperusha vyema bendera ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi nchini.